# NyotaStar Bible School

*Chuo cha Biblia na Afya*

## Kitabu cha Mwongozo kwa Wanafunzi

*Student Handbook*

Changanua kufungua tovuti
**nyotastar.org/sw**

Ugweno, Wilaya ya Mwanga · Mkoa wa Kilimanjaro, Tanzania
contactus@nyotastar.org · nyotastar.org

TOLEO LA KWANZA · 2026

# Yaliyomo

*Contents*


1 Karibu *Welcome* 3
2 Kuhusu NyotaStar *About NyotaStar* 3
3 Kozi *The course* 4
4 Nani anaweza kujiunga *Who may join* 4
5 Jinsi ya kuomba *How to apply* 5
6 Tunachokuomba *What we ask of you* 5
7 Maisha ya kila siku na kila wiki *Daily and weekly life* 6
8 Sabato *The Sabbath* 7
9 Chakula *Meals* 7
10 Kazi shambani na kituoni *Work on the land and around the campus* 8
11 Makazi *Where you live* 8
12 Mavazi *Dress* 9
13 Simu, intaneti na muziki *Phones, internet and music* 9
14 Kutoka nje ya kituo, wageni na familia *Leaving campus, visitors and family* 10
15 Mahusiano *Relationships* 10
16 Wanandoa na familia *Married students and families* 10
17 Masomo na cheti *Studies and the certificate* 11
18 Huduma vijijini *Field outreach* 12
19 Afya *Health* 12
20 Pesa *Money* 13
21 Mali ya shule na vifaa *School property and tools* 13
22 Vitu visivyoruhusiwa *Things not allowed* 13
23 Mambo yanapokwenda vibaya *When things go wrong* 14
24 Kutoa malalamiko na ulinzi *Raising a concern – and keeping everyone safe* 14
25 Picha *Photographs* 14
26 Baada ya kozi *After the course* 15
27 Kufika NyotaStar *Coming to NyotaStar* 15
28 Makubaliano yako *Your agreement* 15

# 1 Karibu

*Welcome*

Karibu NyotaStar Bible School. Kwa miezi sita ijayo, bonde hili litakuwa nyumbani kwako, darasa lako na uwanja wako wa huduma.

Umekuja kujifunza kufanya kile alichofanya Yesu: kufundisha, kuhubiri na kuponya. "Naye Yesu alikuwa akizunguka katika miji yote na vijiji, akifundisha katika masinagogi yao, na kuihubiri Habari Njema ya ufalme, na kuponya magonjwa yote na udhaifu wa kila namna" (Mathayo 9:35, SUV).

Kitabu hiki kinaeleza jinsi maisha yanavyoendeshwa NyotaStar, na kwa nini. Tafadhali kisome chote kabla ya kutuma maombi. Katika fomu ya maombi utathibitisha kwamba umekisoma na unakubali kuishi kwa mujibu wake. Tunaomba hivi kwa sababu shule ya watu arobaini wanaoishi, kufanya kazi na kuomba pamoja inaweza kwenda vizuri tu pale kila mmoja anapojua kilichokubaliwa.

Kama kuna jambo lisiloeleweka, uliza kabla ya kuja. Andika kwa contactus@nyotastar.org.

# 2 Kuhusu NyotaStar

*About NyotaStar*

NyotaStar ilianzishwa mwaka 2004 katika bonde la Ugweno, milima ya Upare Kaskazini, wilaya ya Mwanga, mkoa wa Kilimanjaro. Ilianza kama kituo cha kuwatunza watoto yatima na wajane wa bonde hili. Leo ni shule inayowaandaa wengine kufanya kazi hiyo.

NyotaStar ni huduma inayojitegemea inayoshirikiana na Kanisa la Waadventista Wasabato, na ni sehemu ya mtandao wa LIGHT wa shule za mafunzo ya uinjilisti wa afya.

Kituo kiko umbali wa dakika 20 kutoka Kifaru, dakika 45 kutoka mji wa Mwanga, na saa moja na nusu kutoka Moshi. Asubuhi kukiwa na anga safi, unauona Mlima Kilimanjaro ng'ambo ya tambarare.

**Dhamira yetu.** NyotaStar inawaandaa wanaume na wanawake kufundisha, kuhubiri na kuponya kama Yesu alivyofanya, na kupeleka Injili, ujumbe wa afya na msaada wa vitendo katika vijiji vya Tanzania.

## 3 Kozi

*The course*

Kozi inachukua miezi sita, na ni ya bweni: utaishi kituoni muda wote. Tarehe za kila kozi hutangazwa kwenye nyotastar.org na kwa makanisa.

Kozi ina sehemu nne:

- **Biblia na uinjilisti.** Sehemu hii inaendelea kozi nzima. Utaanza kuhubiri katika wiki za mwanzo, kwa sababu kuhubiri hujifunzwa kwa kuhubiri.
- **NyotaStar Nuru.** Mwezi mmoja wa uinjilisti wa afya kwa mtaala wa LIGHT: kuhudumia magonjwa ya kawaida, tiba rahisi za asili, lishe na mapishi, na kuendesha programu ya afya katika kanisa la kijijini.
- **Huduma vijijini.** Wiki tatu vijijini: mafundisho ya Biblia majumbani, huduma ya afya, na kazi za vitendo za kusaidia jamii.
- **Shamba.** Utajifunza kuotesha miche, kuweka matandazo, kumwagilia na kupanda. Mashamba yanalisha jiko la shule, kwa hiyo kazi yako shambani ndiyo chakula kilicho kwenye sahani yako.

Mafunzo ya afya yanasaidia huduma ya kitabibu, hayachukui nafasi yake. Unajifunza kutambua jambo linalohitaji kliniki, na kuwapeleka watu huko.

**Unachojifunza:**

- **Mafundisho na unabii:** imani za Kanisa la Waadventista Wasabato, Danieli na Ufunuo, patakatifu
- **Uinjilisti na kuhubiri:** uinjilisti binafsi, kutoa mafundisho ya Biblia, uinjilisti wa hadhara, kuhubiri
- **Maisha ya Kikristo na nyumbani:** maisha ya Kikristo, nyumba ya Kikristo, elimu ya kweli, uwakili
- **Roho ya Unabii na historia:** karama ya unabii, historia ya kanisa na historia ya Waadventista

Mafundisho yanatolewa kwa **Kiswahili na Kiingereza**, pamoja na tafsiri inapohitajika.

Wiki za mwezi wa Nuru na za huduma vijijini hutangazwa pamoja na kila kozi.

## 4 Nani anaweza kujiunga

*Who may join*

Unatakiwa:

- kuwa **mshiriki aliyebatizwa wa Kanisa la Waadventista Wasabato**, mwenye msimamo mzuri
- kujua **kusoma na kuandika** Kiswahili au Kiingereza. Hakuna cheti cha shule kinachohitajika.
- kuja na nia ya kumtumikia Mungu na watu wengine baada ya kozi

**Chini ya miaka 18?** Unahitaji ruhusa ya wazazi wako ili kujiunga. Mzazi lazima awasiliane na mkurugenzi kabla hujatuma maombi.

**Wanandoa na wazazi** — angalia sehemu ya 16.

## 5 Jinsi ya kuomba *How to apply*

1. Jaza **fomu ya maombi**. Iko kwa Kiingereza na Kiswahili. Andika kwa herufi kubwa, kwa kalamu ya wino mweusi au wa bluu.
2. Chagua **wadhamini watatu**: mchungaji wako, kiongozi wa kanisa, na mtu mwingine mmoja anayekufahamu vizuri. Mpe kila mmoja **fomu ya mapendekezo**. Wao wenyewe wataituma chuoni, si kupitia kwako, ili waandike kwa uhuru.
3. Tuma fomu yako ya maombi **kwa barua pepe** (contactus@nyotastar.org) au **kama picha iliyo wazi kwa WhatsApp**. Namba ya WhatsApp iko kwenye nyotastar.org.
4. Mkurugenzi atakupigia simu kwa **mahojiano mafupi**.

Fomu inauliza kuhusu kanisa lako, elimu yako, lugha unazozungumza, kusoma na kuandika, ujuzi wako wa kazi za mikono, na afya yako. Unachoandika kuhusu afya yako kinatumika tu kukuhudumia ukiwa chuoni, na kinahifadhiwa kwa siri.

Mwishoni mwa fomu unathibitisha kwamba ulichoandika ni kweli, na kwamba umesoma kitabu hiki na unakubali kuishi kwa mujibu wake.

**Maombi hufungwa mwezi mmoja kabla ya kozi kuanza.** Utapata jibu ndani ya wiki mbili baada ya mahojiano yako.

Maombi yaliyokamilika tu ndiyo yanashughulikiwa: fomu, pamoja na fomu zote tatu za mapendekezo.

## 6 Tunachokuomba *What we ask of you*

Kwa kuja NyotaStar unakubali:

- kutenga muda kila siku kwa maombi na kujifunza Biblia, si darasani tu
- kuishi kwa mujibu wa Biblia na mafundisho ya Kanisa la Waadventista Wasabato
- kuhudhuria darasa, ibada na kazi kwa wakati, na kumaliza kazi unayopewa
- kuiona kazi ya mikono kuwa sehemu ya elimu yako, si mapumziko kutoka kwayo
- kuutunza mwili wako mbali na pombe, tumbaku na dawa za kulevya, kwa sababu ni hekalu la Mungu
- kujitunza katika usafi wa kimwili na kimaadili
- kuwa mwaminifu katika kila jambo: katika maneno yako, kazi zako za darasani na fedha
- kuweka mema ya familia nzima ya shule mbele ya matakwa yako binafsi

**Hakuna mizaha wala hila** dhidi ya mtu yeyote. Watendee wengine kama ambavyo ungependa wakutendee, na badala yake tafuta matendo madogo ya upendo.

# 7 Maisha ya kila siku na kila wiki

*Daily and weekly life*

Ratiba ya kudumu ya kila siku inawawezesha watu arobaini kushiriki vyumba, jiko na mashamba yale yale bila vurugu. Pia inalinda usingizi wako, ambao utauhitaji.

| | |
|---|---|
| **11:30 alfajiri** | Kengele ya kuamka |
| **11:45–12:30** | Ibada binafsi |
| **12:30–1:00 asubuhi** | Ibada ya asubuhi |
| **1:00–1:40** | Kifungua kinywa |
| **2:00–6:30** | Masomo |
| **6:30–7:30 mchana** | Chakula cha mchana na mapumziko |
| **8:00–11:00 jioni** | Kazi shambani na kituoni |
| **11:00–12:30** | Muda binafsi, kuoga na kufua |
| **12:30–1:00 usiku** | Chakula chepesi cha jioni |
| **1:00–1:45** | Ibada ya jioni |
| **1:45–3:00** | Kujisomea |
| **3:30 usiku** | Kuzima taa |

**Wiki.** Masomo ni **Jumatatu hadi Alhamisi, na Ijumaa asubuhi**. Ijumaa mchana ni kwa ajili ya kujiandaa kwa Sabato.

**Jumapili** ni siku ya mapumziko: kufua nguo, kujisomea, muda binafsi, na ziara za familia (angalia sehemu ya 14).

**Mkutano wa maombi** ni **Jumatano jioni**, badala ya ibada ya jioni.

Mtapokezana kuongoza ibada ya asubuhi au ya jioni. Ratiba itabandikwa.

Mara moja kwa mwezi, wanafunzi wote na watumishi hukutana pamoja kuzungumza kuhusu maisha ya chuoni: yanayokwenda vizuri, yanayohitaji kubadilika, na yanayokuja.

**Lugha chuoni.** Chuoni tunazungumza **Kiswahili au Kiingereza**, ili kila mmoja amwelewe mwenzake. Vijijini unaweza kutumia lugha ya mahali ili kuwafikia watu.

**Burudani.** Burudani hapa si ya mashindano: matembezi milimani, kuimba pamoja, mazoezi ya asubuhi, na matembezi mafupi baada ya kula.

## 8 Sabato

*The Sabbath*

Sabato huanza jua linapozama Ijumaa hadi jua linapozama Jumamosi. Ugweno jua huzama karibu saa 12:30 jioni mwaka mzima.

**Mahali pa ibada.** Baadhi ya Sabato mnaabudu pamoja hapa chuoni. Nyingine mnakwenda katika makanisa ya vijiji vya jirani. Ratiba itabandikwa.

**Maandalizi ya Ijumaa.** Kabla jua halijazama Ijumaa, nguo zako ziwe zimefuliwa na kukauka, chumba chako kiwe safi, na jikoni kiwe kimepikwa kile kinachoweza kupikwa mapema.

**Wakati wa Sabato.**

- Unahudhuria ibada ya kukaribisha Sabato Ijumaa jioni, Shule ya Sabato na ibada kuu.
- Hakuna kununua wala kuuza, hakuna kazi shambani, hakuna kujisomea kwa ajili ya mitihani, wala muziki au burudani za kidunia.
- Mchana wa Sabato ni kwa ajili ya mapumziko, kufurahia uumbaji, kuwatembelea wagonjwa, na huduma.

Kazi fulani haziwezi kusimama siku ya Sabato: kugawa chakula, kuosha vyombo, kumhudumia mgonjwa, na kuwalisha na kuwanywesha mifugo. Kazi hizi hufanywa kwa zamu, na ni zile za lazima tu.

## 9 Chakula

*Meals*

Shule inafuata mlo wa **mboga (vegetarian)**: bila nyama wala samaki. Mayai na maziwa yanatolewa. **Chai na kahawa** havitolewi.

**Wanafunzi wanapika kwa zamu.** Kupika ni sehemu ya unachojifunza hapa, na ni sehemu ya mafunzo ya afya ya Nuru.

**Milo miwili kwa siku na chakula chepesi cha jioni:** kifungua kinywa saa 1:00 asubuhi, chakula cha mchana saa 6:30 mchana, na chakula chepesi saa 12:30 jioni.

Jiko haliwezi kuandaa chakula maalumu kwa mwanafunzi mmoja mmoja. Kama una mzio wa chakula au unatakiwa kufuata mlo maalumu kwa sababu za kiafya, liandike katika sehemu ya afya ya fomu ya maombi ili tulizungumze kabla hujaja.

Hakuna chakula ndani ya vyumba vya kulala. Chakula huleta panya na wadudu.

Chukua sehemu yako tu, ili kila mtu apate. Kula mahali chakula kinapogawiwa, si sehemu nyingine za kituo.

## 10 Kazi shambani na kituoni

*Work on the land and around the campus*

Kazi ni sehemu ya kozi, si nyongeza. Unajifunza kilimo kwa kulima, na mashamba yanalisha jiko.

**Muda wa kazi** ni **Jumatatu hadi Alhamisi mchana**, saa tatu, kuanzia saa 8:00 hadi 11:00 jioni.

**Kazi zenyewe:** shamba na bustani (miche, kupanda, kupalilia, kumwagilia, kuvuna), jikoni, kuhudumia mifugo, na ujenzi na matengenezo.

Msimamizi wako atazungumza nawe kuhusu kazi yako kila mwezi. Kama kazi yako itaendelea kuwa ya uzembe hata baada ya kuongeleshwa, hilo litazingatiwa katika uamuzi kuhusu cheti chako.

**Kuzunguka mabweni**, wanafunzi hushirikiana kazi za kila siku kwa zamu: kukata kuni, kubeba maji, kusafisha bafu na vyoo, kukata nyasi na kuweka mazingira safi.

## 11 Makazi

*Where you live*

Wanaume na wanawake wanalala katika **majengo tofauti**. Wanaume hawaingii jengo la wanawake, na wanawake hawaingii jengo la wanaume. Hili linamlinda kila mtu, pamoja na wewe.

**Shule inatoa** kitanda na godoro, chandarua, blanketi na mashuka.

Vyumba ni **mabweni** ya wanafunzi sita au zaidi.

Unalala kwenye kitanda ulichopangiwa tu.

**Usafi.** Unasafisha chumba chako mwenyewe kila siku. Vyumba vya pamoja, vyoo na sehemu za kuogea husafishwa kwa zamu.

**Unaoishi nao chumbani.** Usitumie wala kuazima vitu vya mwenzako bila kumwomba. Punguza sauti yako na ya simu wengine wanapohitaji utulivu. Waombee unaoishi nao chumbani.

**Mali zako.** Hakuna masanduku ya kufunga, kwa hiyo weka pesa na simu yako karibu nawe. Shule haiwezi kuwajibika kwa vitu vilivyopotea au kuibwa. Kitu chochote kitakachoachwa zaidi ya siku 30 baada ya kozi kwisha kitatolewa kwa wengine.

**Tunza maji na umeme.** Zima taa usizotumia, na tumia maji kwa uangalifu.

## 12 Mavazi

*Dress*

Mavazi yako ni sehemu ya ushuhuda wako. Watu wa vijijini watauhukumu ujumbe kwa kumtazama mjumbe.

- Vaa kwa staha, kwa unadhifu na kwa urahisi — si kwa uzembe wala kwa majivuno.
- Darasani, ibadani na katika huduma: wanawake huvaa sketi au magauni yanayoshuka chini ya magoti; wanaume huvaa suruali na shati lenye kola.
- Shambani: nguo za kazi na viatu imara au buti za mpira.
- Hakuna nguo zisizo na mikono, nguo zinazoonyesha mwili, nguo zinazobana, wala shingo za wazi.
- Hakuna mapambo ya vito wala vipodozi vya rangi.

Kama huna uwezo wa kubadilisha mavazi yako, tuambie kabla ya kuja. Tungependa kukusaidia kuliko kukukataa.

**Mapambo ya vito hayavaliwi, pamoja na pete za ndoa.** Kama umeoa au umeolewa, unakaribishwa kuzungumza na mkurugenzi kuhusu hili kabla ya kutuma maombi.

**Mwonekano.**

- Nywele ziwe safi na nadhifu, na za rangi yake ya asili. Wanaume hunyoa nywele fupi. Ndevu, kama unazo, zitunzwe kwa unadhifu.
- Hakuna rangi ya kucha wala midomo, kwa wanaume na wanawake.
- Kama una chanjo (tattoo) mwilini, ifunike pale inapowezekana.

## 13 Simu, intaneti na muziki

*Phones, internet and music*

**Unabaki na simu yako**, hata usiku. Unaweza **kuichaji** chuoni, na kuna **intaneti** kituoni.

Simu **huzimwa ibadani**. **Darasani**, unaweza kutumia simu kama Biblia au kwa kuandika kumbukumbu ikiwa kwenye **hali ya ndegeni (airplane mode)**. Hupokei simu wala kujibu ujumbe darasani.

Hakuna filamu, tamthilia wala video za burudani kituoni. Muziki uwe wa kiroho, unaoendana na Wafilipi 4:8. Tumia vifaa vya masikioni, au waombe kwanza unaoishi nao chumbani.

Tumia simu na intaneti kwa uaminifu. Usifungue chochote ambacho usingekifungua mbele ya mwalimu wako.

**Hakuna michezo ya video au ya kompyuta** kwenye kifaa chochote ukiwa mwanafunzi.

## 14 Kutoka nje ya kituo, wageni na familia *Leaving campus, visitors and family*

**Rudi kabla ya saa 1 usiku.** Uwe kituoni kabla ya saa moja jioni (19:00), kabla ya ibada ya jioni.

**Kulala nje** kunahitaji ruhusa ya **mkurugenzi**.

**Ziara za familia** ni siku ya **Jumapili**, kwa kupanga mapema na mkurugenzi.

**Kwenda nyumbani** wakati wa kozi ni kwa **dharura tu**, kama msiba au ugonjwa mkubwa katika familia. Zungumza na mkurugenzi.

Kila unapotoka nje ya kituo, jiandikishe unapotoka na unaporudi. Tunahitaji kujua kila mtu yuko wapi, kwa ajili ya usalama wako.

**Matembezi.** Mara kwa mara shule hupanga matembezi. Kila kilichomo katika kitabu hiki kinahusika pia wakati wa matembezi. Usiende msituni, milimani wala mtoni peke yako, na kila mara mwambie mtu unakokwenda.

**Mawasiliano na familia.** Shule haipokei barua za wanafunzi. Familia yako inawasiliana nawe kwa simu.

**Kutokuwepo bila ruhusa.** Mwanafunzi aliye nje ya chuo bila ruhusa yuko hatarini kufukuzwa.

## 15 Mahusiano *Relationships*

Urafiki kati ya wanaume na wanawake unakaribishwa ukiwa wa kikundi. Uko hapa kujiandaa kwa maisha ya huduma, na uchumba mpya huuvuta moyo mbali na lengo hilo. Kwa sababu hiyo:

- hakuna uchumba wala kutafuta mchumba wakati wa kozi
- hakuna watu wawili kujitenga — kuwa pamoja kila wakati, mbali na kikundi
- uhusiano wowote wa kimwili unasababisha kufukuzwa

Kama wanafunzi wawili wanaamini Mungu anawaongoza kuelekea ndoa, wanazungumza na mkurugenzi. Uchumba unaweza kuanza tu kwa ruhusa ya mkurugenzi.

## 16 Wanandoa na familia *Married students and families*

Wanandoa, na wazazi ambao wangetaka kuja na mtoto, wanaangaliwa **kila mmoja kwa hali yake**. Zungumza na mkurugenzi kabla ya kutuma maombi.

# 17 Masomo na cheti

*Studies and the certificate*

**Mahudhurio.**

- Fika kwa wakati darasani, ibadani, kazini na katika huduma.
- Kuchelewa zaidi ya dakika tano kunahesabiwa kama kutohudhuria. Kuchelewa mara tatu ni sawa na kutohudhuria mara moja.
- Kama huwezi kuhudhuria kwa sababu ya ugonjwa au dharura, mjulishe mwalimu kabla, kama inawezekana.
- Kutohudhuria mara tatu bila sababu ya msingi husababisha onyo. Ukikosa zaidi ya kipindi kimoja kati ya kumi bila sababu ya msingi, hujafaulu somo hilo.

**Darasani.** Hakuna kula darasani. Liache darasa likiwa safi, na uchukue vitu vyako. Kompyuta na simu kwa ajili ya somo tu.

**Kulala darasani** hakukubaliki. Ukijisikia vibaya, mwambie mwalimu wako, naye atakusaidia.

**Uaminifu.** Kunakili kazi ya mtu mwingine au kudanganya katika mtihani kunaweza kusababisha kufukuzwa.

**Jinsi unavyopimwa.** Unapimwa kwa njia nne:

- **majaribio ya maandishi** katika kila somo
- **kuhubiri**: mahubiri yako yanapimwa na walimu wako
- **mitihani ya vitendo**: ujuzi wa afya, upishi na kazi shambani
- **kazi na mwenendo wako**: kazi, maisha bweni, na mahudhurio

**Cheti chako.** Ukimaliza kozi unapata **cheti kimoja** kutoka NyotaStar. Kinahusu kozi ya miezi sita ya Biblia na uinjilisti pamoja na mwezi wa NyotaStar Nuru wa uinjilisti wa afya. Kinatolewa na shule yenyewe.

Ili kupata cheti lazima uwe umefaulu masomo yako na umekamilisha huduma vijijini.

**Mahafali.** Kozi inahitimishwa kwa **ibada ya mahafali**. Familia yako inakaribishwa.

## 18 Huduma vijijini

*Field outreach*

Kwa wiki tatu utakwenda vijijini: mafundisho ya Biblia majumbani, huduma ya afya, na kazi za vitendo za kusaidia jamii. Hapa ndipo unapotumia kile ulichojifunza.

**Mahali pa kukaa.** Washiriki wa makanisa ya vijijini wanawapokea na kuwakaribisha. **Shule inalipia usafiri** wa kwenda vijijini na kurudi.

**Wawili wawili.** Mnafanya kazi wawili wawili, chini ya uongozi wa mwalimu au mfanyakazi wa Biblia mwenye uzoefu. Unakwenda na mwenzako, kamwe si peke yako.

"Baada ya hayo Bwana aliweka wengine, sabini, akawatuma wawili wawili, wamtangulie kila mji na mahali alipokuwa yeye mwenyewe atakaribia kufika." (Luka 10:1, SUV)

Mwanamume na mwanamke hawaendi wawili peke yao. Hili linakulinda wewe, watu mnaowatembelea, na jina la shule.

Kila kilichomo katika kitabu hiki kinahusika pia vijijini: mavazi, Sabato, mahusiano, simu. Ukiwa kijijini, wewe ndiye shule.

Mtu akiwa mgonjwa, unamsaidia kufika kliniki. Mafunzo ya afya yanasaidia huduma ya kitabibu, hayachukui nafasi yake.

**Vitabu na vyombo vya habari.** Kabla ya kugawa vitabu, vijitabu, CD, video au flash yoyote, watumishi lazima wavikubali kwanza.

## 19 Afya

*Health*

Unachoandika kuhusu afya yako kwenye fomu ya maombi kinatumika tu kukuhudumia ukiwa hapa. Kinahifadhiwa kwa siri. **Hakuna fomu nyingine ya afya inayohitajika.**

**Bima ya afya.** Unapata bima kupitia **NHIF**, inayolipiwa kutoka kwenye TSh 400,000 unazotuma kabla ya kozi (angalia sehemu ya 20).

**Ukiugua**, mjulishe mkurugenzi mara moja. Utapelekwa **zahanati iliyo karibu katika bonde**. Kwa jambo kubwa zaidi, unakwenda **Hospitali ya Wilaya ya Mwanga**.

Kwa matatizo madogo shule inatoa huduma ya kwanza na tiba rahisi za asili. Shule haina daktari, na si hospitali.

Dawa unazotumia kila siku: leta za kutosha miezi sita.

## 20 Pesa *Money*

**Hakuna ada ya masomo.** Mafunzo, malazi na chakula chako vinatolewa. Vinagharamiwa na watu wanaokisaidia chuo.

**Unatuma TSh 400,000 kabla ya masomo.** Ni kwa ajili ya vifaa vyako vya masomo, bima yako ya afya na matumizi yako binafsi. Chuo kinakutunzia na kinazitumia gharama hizo zinapotokea. **Ni pesa zako, si ada.**

**Nauli ni juu yako.** Unalipia safari yako ya kuja chuoni na ya kurudi nyumbani. Ukihitaji msaada wa safari, weka alama kwenye kisanduku cha fomu ya maombi na utuambie.

**Ukiondoka mapema**, kwa sababu yoyote ile, kiasi ambacho hakijatumika **kinarudishwa**: kwako, au kwa mtu aliyetuma pesa hizo kwa ajili yako. Utazihitaji kwa safari ya kurudi nyumbani.

**Taarifa ya matumizi.** Hakuna kiasi maalumu cha pesa za matumizi binafsi. Shule inaandika kinachotumika kwa vifaa vyako na bima yako ya NHIF, na kinachobaki ni chako kutumia.

**Kutuma pesa.** TSh 400,000 zifike **wiki mbili kabla ya kozi**, kwa benki au pesa kwa simu. Maelezo yanakuja pamoja na barua yako ya kukubaliwa.

Unaweza kuomba wakati wowote kuona kiasi kilichotumika kutoka kwenye pesa zako, na kwa ajili ya nini.

**Usikope pesa** kwa watumishi wala kwa wageni, wawe Watanzania au kutoka nje. Ukiwa na hitaji, la pesa au jingine lolote, zungumza na mwalimu anayekuhusu, na yeye tu.

## 21 Mali ya shule na vifaa *School property and tools*

Vifaa huandikishwa unapovichukua na hurudishwa vikiwa safi kabla ya siku kwisha. Kifaa kilichoachwa shambani hushika kutu au hupotea, na hapo mwingine anakosa cha kufanyia kazi.

Usipigilie misumari wala kubandika chochote ukutani au kwenye samani. Usihamishe samani.

**Uharibifu.** Ukiharibu kitu kwa uzembe, unalipa **hadi nusu** ya gharama ya matengenezo.

**Gari la shule.** Huliendeshi bila ruhusa na leseni halali ya udereva.

## 22 Vitu visivyoruhusiwa *Things not allowed*

Vitu hivi haviruhusiwi kituoni, wakati wa huduma, wala mahali popote ukiwa mwanafunzi:

- pombe, tumbaku, bangi au dawa nyingine yoyote ya kulevya
- chai, kahawa na vinywaji vingine vyenye kafeini
- silaha za aina yoyote
- picha au video za ngono
- hirizi au kitu chochote kinachotumika katika uchawi

Kuleta au kutumia kitu chochote kati ya hivi husababisha kufukuzwa mara moja.

## 23 Mambo yanapokwenda vibaya *When things go wrong*

Tunataka kukusaidia ubaki, si kutafuta sababu za kukuondoa. Mwanafunzi anapokwenda kinyume na yaliyokubaliwa, tunaanza kwa mazungumzo na maombi.

1. Kwanza, angalau maonyo mawili ya mdomo. Kila onyo linaandikwa.
2. Kama hakuna mabadiliko, onyo la maandishi kutoka kwa **mkurugenzi na kamati ya watumishi**.
3. Kama bado hakuna mabadiliko, **mkurugenzi pamoja na kamati ya watumishi** wanaamua kama utaondoka kwenye kozi.

**Kufukuzwa mara moja.** Kwa makosa makubwa, hatua hizo zinaweza kurukwa: vurugu, utovu wa maadili ya kingono, wizi, pombe au dawa za kulevya, kitu chochote cha sehemu ya 22, au kumdhuru mtoto au mtu aliye hatarini.

**Rufaa.** Ukifukuzwa, unaweza kuomba uamuzi huo upitiwe upya na **mchungaji wa mtaa wa Kanisa la Waadventista Wasabato** wa eneo hili. Mwandikie **ndani ya siku 7** baada ya uamuzi.

## 24 Kutoa malalamiko na ulinzi *Raising a concern – and keeping everyone safe*

Una haki ya kuwa salama hapa. Mtu akikutendea vibaya, au ukiona jambo baya, tuambie. Hakuna mwanafunzi atakayeadhibiwa kwa kutoa malalamiko kwa uaminifu.

Unaweza kuzungumza na:

- mkurugenzi: ____________________
- mwanamke miongoni mwa watumishi, kwa jambo lolote ambalo mwanamke angependa kulieleza kwa mwanamke: ____________________
- mtu aliye nje ya uongozi wa kila siku wa shule, kama malalamiko yako yanamhusu mtumishi: ____________________ simu: ____________________

Kama huenda kosa la jinai limetendeka, shule itakusaidia kuripoti polisi, na haitalinyamazia ili kulinda jina lake.

Hakuna mtumishi wala mwanafunzi atakayekaa peke yake na mtoto, au na mwanafunzi wa jinsia nyingine, nyuma ya mlango uliofungwa.

## 25 Picha *Photographs*

Kwenye fomu ya maombi unaweza kukubali hili:

"Picha zangu za chuoni zinaweza kutumika kwenye tovuti na machapisho ya chuo. Naweza kuondoa ruhusa hii wakati wowote kwa maandishi."

Usipoweka alama, hatutatumia picha ambazo unaweza kutambulika. Ukiweka alama kisha ukabadili nia, mwandikie mkurugenzi, nasi tutaacha kuzitumia.

Tafadhali usiweke mtandaoni picha za wanafunzi wenzako au za watu mnaowatembelea vijijini bila kuwaomba kwanza.

## 26 Baada ya kozi

*After the course*

Kozi inakuandaa kwa huduma katika kanisa na jamii yako. Shule haikuahidi kazi baadaye.

Pale inapowezekana, shule inawaunganisha wahitimu na makanisa na huduma zinazotafuta watenda kazi.

## 27 Kufika NyotaStar

*Coming to NyotaStar*

**Jinsi ya kufika.** Nauli ni juu yako (angalia sehemu ya 20). Kutoka Moshi ni takriban saa moja na nusu hadi chuoni. **Ukifika Mwanga, piga simu chuoni.** Tutakuambia mahali hasa pa kushuka kwenye basi.

**Siku ya kuwasili.** Fika **siku moja kabla masomo hayajaanza, kabla ya saa 10:00 jioni**, na ujiripoti kwa mkurugenzi.

Tafadhali usifike kabla ya siku ya kuwasili. Vyumba havitakuwa tayari.

**Vitu vya kuleta.**

- Biblia (ya Kiswahili, na ya Kiingereza kama unayo), na vitabu vyako vya Roho ya Unabii
- daftari, kalamu
- mto wa kulalia
- nguo za darasani na ibadani, nguo za kazi, viatu imara au buti za mpira
- sweta — usiku milimani Upare kuna baridi. Vifaa vya kulalia vinatolewa (angalia sehemu ya 11).
- sabuni, taulo, ndoo, tochi
- dawa unazotumia kila siku, za kutosha miezi sita
- kitambulisho chako na **picha mbili za pasipoti**, za kukabidhi unapowasili

**Vitu vya kutoleta.** Vitu vya thamani usivyovihitaji, redio au televisheni, na chochote kilichoorodheshwa katika sehemu ya 22.

**Wanafunzi kutoka nje ya Tanzania.** Wasiliana na shule kabla ya kutuma maombi, ili kuzungumza kuhusu kibali utakachohitaji.

## 28 Makubaliano yako

*Your agreement*

Unapoweka alama kwenye kisanduku cha fomu ya maombi, unasema:

"Nimesoma kitabu hiki chote. Nimekielewa, na ninakubali kuishi kwa mujibu wake nikiwa mwanafunzi wa NyotaStar."

Kama kuna jambo lolote usiloweza kukubali, zungumza nasi kabla ya kutuma maombi.

**Unapowasili** unasaini ahadi iliyo hapa chini na kuikabidhi kwa mkurugenzi.

**Ahadi · Commitment**

Nimesoma kitabu hiki, na ninakubali kuishi kwa mujibu wake nikiwa mwanafunzi wa NyotaStar.

| Jina | Sahihi | Tarehe |
|---|---|---|
| | | |